# SALA YA KUWAOMBEA MAPADRE

Na Stanslaus Butungo,
Chuo cha misitu-SUA: Olmotonyi, ARUSHA
25th March 2014

Taratibu na kwa moyo wa Ibada.







2. Ewe Roho Mtakati-fu, ndiwe tunda-la uadili-fu,
Kiongozi wa kiro-ho, na zawadi- ya Mwokozi we-tu
Wajalie tunu ya usa-fi, uwakinge na adui mba-ya
Wahifadhi kwenye moyo wa- Yesu, wasicha-fu-ke mioyo yao.

3. Kwa unye-nyekevu mku-u, tunaomba- kwako Bwana mwema,
Kwa uwe-zo wa peke-e, na Umungu- wako wa aja-bu.
Katika upweke wafari-ji, waongoze hata kwenye ho-fu,
Wajalie watambue kwa-mba, kwa mateso roho za safi-shwa

4. Hata si-si wana wako, tusiosta-hili mbele ya-ko.
Tujali-e- kuwape-nda, na kuwatunza makasisi we-tu
Tusiwa-ka-ti-she tamaa, wanapo-fa-nya- kazi ya-ko,
Kwani kwa nji-a- ya mapa-dre ndipo tu-na-pa-ta woko-vu.

5. Ee Maria, Mtakatifu, ndiwe mama-wa mapadre we-tu
Yesu a-likukabi-dhi alipokuwa m-salaba-ni.
Waombee tunu ya utii, ubikira na umasiki-ni,
Waongoze ili watuo-ngoze, kwenye makao ya milele. AMINA

+255 752 580 252 na +255 714 896 623
E mail: butungo@yahoo.com/butungo@gmail.com

**Mapadre ni tunu bora sana aliyotuachia Bwana Yesu.**
**Hutuunganisha na mbingu kwa njia ya sakramenti. Tuwatunze, tuwaombee na tusiishie kuwahukumu**